


Haki ya Msingi ya Usawa mbele ya Sheria.

TAWLA ipo kwa kukusaidia wewe kuelewa nini hasa maana ya Haki hii.

Endapo una swali lolote, au unahitaji msaada, tafadhali tuandikie "TAWLA", S.L.P. 9460, Dar es Salaam Tanzania.



DESIGN NA MICHORO WALTER LEMA
(DESIGN AND DRAWING)
REDISIGN HELMUT PFINDEL

IMEFADHILIWA KWA PAMOJA
NA ROYAL DANISH EMBASSY
IMEFADHILIWA NA MEDICAL MISSION SUPPORT
UNITED STATES INFORMATION SERVICES (USIS)

KUTENGANA AU TALAKA



IMETOLEWA NA KUTAYARISHWA NA CHAMA CHA
WANAWA KE WANASHERIA TANZANIA (TAWLA)

KUTENGANA AU TALAKA

Ili uweze kutengana au kuomba talaka lazima kuwepo ndoa inayotambulika kisheria.

Aina za ndoa; (Sheria ya ndoa ya mwaka 1971)

1. Ndoa ya mke mmoja au zinakusudiwa ziwe za mke mmoja
2. Ndoa za mitara (za wake wengi) au zinazoweza kuwa za mitara (wake wengi).

Ndoa zinaweza kufungwa kama ifuatavyo:

- (a) Kiserikali au
- (b) Kiserikali au iwapo mnafunga ndoa wote wawili ni watu wa dini moja iliyotajwa, inaweza kufungwa kwa mujibu wa desturi na dini hiyo;
- (c) Kiserikali au kwa dini ya Kiislamu ikiwa mume anayekusudwa ni Muislam; au
- (d) Kiserikali au kwa mujibu wa kanuni za Sheria ya mila iwapo wafunga ndoa hao ni wa jamii moja au wa jamii mbalimbali zinazofuatwa kwa sheria za mila.

DHANA YA NDOA

- Iwapo itathibitika kwamba mwanamume au mwanamke wameishi pamoja kwa miaka miwili au zaidi katika hali ya kuweza kupata heshima ya mke na mume basi itatungwa hoja inayoweza kubishaniwa kwamba watu hao walioana ipasavyo.

Dhana hii ikikubalika na mahakama mwanamke huyo atakuwa na haki ya kupata masurufu yake na ya mtoto na muungano huo baada ya hukumu ya kuvunja ndoa au hukumu ya kutengana.

KUTENGANA

Kutengana ni hali ya kutaka ndoa isivunjike moja kwa moja bali mume na mke wanaishi mbali mbali kwa muda ambao kawaida ni miaka miwili au mitatu.

Madhumuni ni kumwezesha mume na mke mwenye kusababisha maudhi kujisahihisha. Pia mwenye kuudhika anapata fursa ya kutulia.

Ombi la kutengana.

- (a) kwa mapatano ya mume na mke na wao wenyewe kwa hiari yao huweza kupanga mipango ya ulinzi na matunzo ya watoto.
- (b) kufikishwa mahakamani na hatimaye mahakama hutoa amri ya kutengana. Ombi la kutaka amri ya kutengana kufikishwa mahakamani moja kwa moja bila kupitia kwenye baraza la usuluhishi.

TALAKA

Maudhi katika ndoa yanaweza kuwa mazito sana na ndipo mlalamikaji mume au mke anapokwenda mahakamani kudai amri ya kuvunja ndoa kabisa ambayo inaitwa amri ya talaka.

Sheria ya ndoa ya mwaka 1971 inasema ya kuwa mashauri ya kudai talaka ambavo lazima yatolewe na mahakama yanapaswa kwanza kupitia kwenye baraza la usuluhishi. Mabaraza ya usuluhishi yapo mengi na yameundwa kwa shughuli hiyo kwenye vijiji na mijini. Jukumu la mabaraza hayo ni kuwasuluhisha mlalamikaji na mlalamikiwa ili waweze kusameheana. Baraza hilo linaposhindwa kusuluhisha, hawana budi kutoa shahada kwa

mume na mke wanaohusika. Shahada hiyo itamwezesha mlalamikaji kufungua madai ya talaka kwenye mahakama. Bila shahada hiyo madai hayawezi kupokelewa mahakamani. Sababu zinazoweza kufanya ndoa ivunjike.

- (a) Maasi au utoro wa makusudi usiopungua miaka mitatu.
- (b) Mlalamikiwa kufungwa jela kwa muda wa miaka mitano mfululizo au maisha.
- (c) Kutengana kwa hiari au kwa amri ya mahakama kusikopungua miaka mitatu.
- (d) Ukatili wa mwili au akili kwa watoto wa ndoa au kwa mlalamikaji.
- (e) Kichaa kinachothibitishwa na madaktari wawili kwamba hakiponi.
- (f) Mlalamikaji kubadili dini ikiwa wote walikuwa na dini moja wakati wa kuoana.

Kwa mujibu wa dini hiyo kubadili dini kunavunja ndoa au kunakuwa na sababu za kuvunja ndoa.

Pamoja na sababu zote hizo hapo juu mahakama itatoa amri ya talaka kama upo ushahidi wa kutosha kuthibitisha kwamba ndoa imevunjika na ndoa hiyo, kwa vyovyote vile haitengemai tena.